**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

**KUMB. NA. AB.285/294/01/76** **19/12/2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasikazi nne (04) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II - NAFASI 04

### 1.1 MAJUKUMU NA KAZI

i. kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na za siri
ii. kupokea wageni na kuwasaidia shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
iii. kutunza taarifa za kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine
iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi
v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Idara/Kitengo sehemu husika
vi. Kukusanya, kutunza na kuyarekebisha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika
vii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali
viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi
ix. Kufanya kazi nyingine atakayoelekezwa na msimamizi wake

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha NNe (Form IV) au cha Sita (Form VI), wenye stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha (NTA Level 6) ya uhazili. Aida wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata program za kompyuta za Ofisi kama vile; Word, Excel, Powerpoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS C**

### MASHARTI YA UJUMLA

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye Umri wa miaka 18 na usiozizdi miaka 45

**ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuhainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa umma.**

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza Curriculum Vitae (CV) yenye Anuani inayotumika,. Namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
“Provisional”/Testimonials”/”Statement of result” na hati za matokeo za kidato cha Nne na Sita (Form Iv and Form VI results slip) **HAVITAKUBALIWA**.

iv. Waombaji wote waambatinishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.

v. Waombaji waliostaafishwa katika utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

vi. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wana na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.

vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma, wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba 2010.

viii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

ix. Postgraduate,Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI,- computer Certificate,- Vyeti vya Kitaaluma ( Professional Certifiacate from REspective Boards).

x. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA au NECTVET).

xi. Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria

xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kingereza.

xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 01 Januari, 2026.

xiv. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya Igunga,**
**S.L.P 19,**
**IGUNGA.**

xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kieletroniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz. Anuani hii pia inapatikana kwenye Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingiza sehemu iliyoandikwa “Recruitment Portal”

xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKILIWA.

Limetolewa na :

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WIALAYA YA IGUNGA**